Mageni ni gani kuhusu Mashauri na Mapimo ya HIV?

Vituo Vingine vya Faragha vya Pimo

Serikali ya Ontario hivi majuzi imeamrisha vituo vingine 24 vipeane mapimo ya faragha, na kufikisha jumla ya vituo 50 na kuongeza upatikanaji wa pimo ya faragha ya HIV kwa eneo nyingi za mkoa. Daktari wasio na muda au uzoefu wa kufanya pimo ya HIV wanaweza kuelekeza wagonjwa kwa kituo cha afya cha umma kinachohusika na mambo ya mapenzi au kwa mpango wa faragha wa kupimwa. Wasiliana kupitia namba za moja kwa moja za simu zinazohusika na UKIMWI kwa maelezo juu ya vituo na namba za simu za vituo vya pimo ya faragha 416-392-2437 or 1-800-668-2437;
Simu ya Kifaransa: 1-800-267-7432.

Maeneo ya Faragha ya Pimo ya HIV, Ontario Iko Wapi?

22 ndani ya vituo vya afya vya umma.

16 ndani ya vituo vya afya vya jamii.

4 ndani ya huduma za mkunga(kwa matumizi tuu. ya wahudumiwa wao}.

3 ndani ya vituo vya afya vya mambo ya mapenzi.

5 kwa maeneo mengine- hospitali, kwa nyakala ya vijana, nyakala mbili za watu asili na kundi ya afya ya jamii.

Mapimo Mengine ya Urahisi

Wizara ya Afya na Tunza ya Muda Mrefu inatoa mapimo ya bure kwa vituo vya kutunzwa kwa vituo vya pimo ya faragha, kliniki za umma za afya za mambo ya mapenzi na vituo vya jamii vya afya ambazo zinajitolea kupeana aina hii ya pimo, na pimo kwa kituo cha tunza. Watu wasio na virusi watajua dakika chache tu baada ya kupimwa. Watu wanao patikana kuathirika na virusi katika kituo cha tunza lazma wafanye kipimo cha kuhakikisha kwa kutumia kiwango sanifu cha pimo ya maabara na watahitajika kusubiri mpaka wiki mbili kupata matokeo yao. (Zingatia: muda wa kupokea matokeo ni tofauti eneo mbali mbali mkoani.) Kuongezea, maabara ya umma ya afya sasa inafanya mapimo ya kidesturi ya p24 ya antigen kwa sampuli yoyote ambayo fomu ya mahitaji inaashiria kwamba mtu yuko kwa kipindi husika, na ana dalili NA amekua na mfichuo wa hatari wa juu.

Habari Zaidi juu ya Hatari

Sasa tunajua

- Wanawake wachanga (yani, chini ya miaka 18) wako hatarini zaidi kuambukizwa na HIV kuliko wanawake wa miaka zaidi kwa sababu selu za mlango wa uzazi hazikui kabisa mpaka miaka 18.
- Afya ya utundo telezi inaathirika na kuwepo kwa ambukizo zingine zinazoletwa na ngono (STIs), viwango vya homoni za mwanamke, kukosa kwa lainisho na utumizi wa vitu vinazowasha.
- Kiwango kidogo cha virusi kinapunguza lakini hakimalizi hatari ya kuambukizwa na HIV. Dawa za kumaliza virusi hasifiki kiwango kikumbwa kinachohitajika mara zote kuangamiza HIV kwenye langa la uzazi. Hatari inaongezeka kama mtu anaathiriwa na ugonjwa mwingine wa ngono.
- Kuna hatari ya kuambikizwa kutokana na kugawana vifaa vingine vya dawa (mbali na sindano), kama jiko, vichuji, maji, vipanguza spiriti, mifundo, mifereji ya dawa za crack na glasi.

Ufahamu Zaidi wa Athiri/Hatari za Jamii

Uwezo wa watu kuendesha na kufanya mapenzi kwa usalama na utumizi wa madawa unaathiriwa na athiri za jamii za afya, kama vile umaskini, mazingira, ukosaji usawa kwa mahusiano, utumiaji wa madawa au pombe na shutumu. Mambo yale yanayo kabili watu mara mingi inageuka kutokana na umri, maelekezo ya mapenzi, utamaduni na rangi.

Ontario

Mashauri ya kuzuia inayofanikiwa lazma ifuatiliye mambo haya yote. (Tazama faharasa ya pili kwa mazungumzo machache ya mambo inayohusika na idadi ya watu.)

Umuhimu wa Kupimwa juu ya Magonjwa Mengine ya Mapenzi na Homa ya Manjano(Hepatitis C)

Watu kiasi ambayo wako hatarini ya kuambikizwa na HIV, wako pia hatarini kwa magonjwa mengine ya mapenzi na hepatitis C. Mtu yoyote anao jitokeza kupimwa kwa HIV anatakiwa pia apewe mawaidha na achunguzwe kwa hatari zingine za magonjwa ya mapenzi na hepatitis C na apewe pimo.

Muda Unaohitajika kwa Pimo ya HIV

Mashauri kabla ya pimo ya HIV yanaweza kufanywa kwa dakika 15 mpaka 20 lakini muda utabadilika kutengemeana na ufahamu wa mhudumiwa na mahitaji mengine.

Sharti ya Kisheria Kueleza Wapenzi wa Baadaye

Miaka michache iliopita, watu kadhaa walio na HIV wamehukumiwa kwa shutumu jinai kwa kuhusika kwa mambo ya mapenzi iliyo na uwezo wa hatari wa kuambukiza HIV bila kueleze wapenzi wao juu ya hali yao ya HIV. Watu wanaopatikana na pimo kuwa na virusi ya HIV lazma sasa washauriwe kueleza wapenzi wao kwamba wana HIV kabla ya kuendeleza shughuli yoyote inayo uwezo wa hatari kama vile mapenzi bila kinga – la hivyo, makubali ya mpenzi ya kufanya ngono si halali na ule mtu aliye na HIV anaweza kustakiwa. Sheria baado si wazi kabisa juu ya mambo mengine ambayo inayo uwezo wa hatari. Kwa habari zaidi juu ya jukumu ya kisheria kueleza hali ya HIV kwa wapenzi wa baadaye, wasiliana na Kliniki ya UKIMWI NA HIV (Ontario) (HALCO): 416-340-7790; 1-888-705-8889; www.halco.org.

Usaidizi na Mambo ya Lugha

Simu ya moja kwa moja kwa mambo ya UKIMWI inatoa habari kwa lugha 18, na ina wafanyikazi waliye na uwezo wa kutoa huduma za kutafsiri na kufasiri wakati washauri hawaongee lugha moja na wahudumiwa. Wanaelewa vyema mambo ya kupimwa kwa HIV na ni rasilimali bora sana. (Namba za moja kwa moja za UKIMWI: 416-392-2437 au 1-800-668-2437; Simu ya Kifaransa: 1-800-267-7432.)

Januari 2008, Simu ya moja kwa moja kwa mambo ya UKIMWI ilipeana huduma kwa lugha zifuatazo:

Kiarmenia
Kibengali
Kicantoni
Kiingereza
Kifilipino
Kifransa
Kihakka
Kihindi
Kimandarin
Kiureno
Kirusi
Kisinhala
Kiispania
Kiswahili
Kitaiwan
Kitamil
Kiurdu
Kivietnam

Usaidizi kwa Kueleza Mpenzi

Ofisi ya UKIMWI inajadiliana na jamii kuzindua maelezo kamilifu zaidi ya kuarifu mpenzi ambayo itasaidia washauri wakabiliane na mambo ngumu.

Vyombo na Orodha Zingine Za Kukaguliwa

Maelezo *ya Mashauri na Pimo ya HIV* ya Wizara ya Afya na Huduma ya Muda Mrefu inajumuisha vyombo kadhaa, kama vile orodha ya kukagua mashauri mbele ya kupimwa, maelezo ya mapenzi kwa usalama kwa njia pesi, dokezo za mashauri na mawaidha ya kupeana matokeo ya pimo inayo ashiria virusi.

Soma zaidi juu ya kupimwa kwa,
SayYesToKnowing.ca

Swahili Catalogue No. CIB-6153431 March/08 © Queen's Printer for Ontario